

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA  
MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA SITA**

121/1

**KISWAHILI 1**

(Kwa Watahiniwa Walioko Shuleni na Wasiokuwa Shuleni)

Muda: Saa 3

Jumatano, 08 Mei 2019 asubuhi

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E zenye jumla ya maswali **kumi (10)**.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A, C na E, maswali **mawili (2)** kutoka sehemu B na swali **moja (1)** kutoka sehemu D.
3. Zingatia maagizo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org



## SEHEMU A (Alama 20)

### UFAHAMU

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Soma kwa umakini kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu kwa usahihi maswali yanayofuata.

Wazo la watu wengi juu ya **muungwana** ni kuwa mtanashati au labda kuwa mtu **arifu** mwenye cheo kwa watu. Lakini nguo nzuri hazimtukuzi mtu wala hazimfanyi kuwa muungwana. Fasili ya hili ni kwamba nguo ni kama ngozi ya mtu au mnyama; au hasa ni duni sana kuliko ngozi au manyoya. Ngozi ya simba haiwezi kumfanya punda kuwa simba. Uungwana wa kufanywa na mshoni ni mzaha; si uungwana wa kweli. Neno muungwana lina maana kubwa zaidi kuliko nguo nzuri au adabu nzuri au elimu nzuri. Kwa hakika twatumia vibaya neno hili kwa mtu yeyote aendaye kwa miguu miwili.

Kwanza muungwana hawezi kumuudhi au kumdhuru mtu kwa maneno au matendo yake, hata kwa kumtazama. Ana moyo wa uvumilivu na anaweza kusikiliza kwa makini maoni ya watu wengine bila ya kujaribu kuwalazimisha wakubali maoni yake. Ni mkarimu, mnyofu na amini katika tabia yake kwa wengine. Hapendi kujionyesha alivyo tajiri au alivyoelimika. Hana makuu wala unafiki, yu mnyofu kwa kila asemalo au atendalo. **Hajitwezi** kwa matendo yake wala hadunishi matendo ya watu wengine kwa sababu hana wivu. Haudhi wala hadhuru mtu yeyote kwa sababu ajua kwamba ushenzi kama huo ni kinyume cha uungwana.

Siku zote muungwana ni mwema kama baba au mama, mwaninifu kama rafiki na msaidizi kama ndugu. Hutenda na tena hujiendesha kama raia **mwadilifu** ajuae kazi na madaraka yake kwa watu. Huchukuana na watumishi wake kwa mapenzi, huruma na upole. Hujiheshimu na kuwaheshimu wengine. Hivyo basi uungwana wake hautokani na malezi ya shule ila hutokana na uungwana wa kweli.

### Maswali

- (a) Andika kichwa cha habari hii.
- (b) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika habari hii.
- (i) Muungwana
  - (ii) Arifu
  - (iii) Hajitwezi
  - (iv) Mwadilifu
- (c) Eleza mawazo makuu mawili ya mwandishi.
- (d) Kutokana na habari uliyosoma, taja tabia tatu za mtu muungwana.
2. Fupisha habari uliyoisoma kwa maneno tisini.

**SEHEMU B (Alama 20)**  
**MATUMIZI YA SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA**  
Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

3. Unaelewa nini kuhusu neno misimu? Kwa kutumia mifano, fafanua njia nne zitumikazo kuunda misimu ya lugha ya Kiswahili.
4. Bainisha mofimu na kisha taja kazi ya kila mofimu katika maneno yafuatayo:
  - (a) Akijikingia
  - (b) Mchezaji
  - (c) Asiyekujua
  - (d) Mmeachiliana
5. (a) Kwa kutumia mifano, fafanua maana ya istilahi zifuatazo:
  - (i) Kielezi
  - (ii) Kiwakilishi
  - (iii) Kivumishi
  - (iv) Kitenzi

(b) Kwa kutumia neno “zuri” tuna sentensi mbili kwa kila aina za maneno yafuatayo:
  - (i) Kielezi
  - (ii) Kiwakilishi
  - (iii) Kivumishi
6. Taja dhima tano za mofimu “KI” katika sarufi kisha tuna sentensi mbili kwa kila dhima.

**SEHEMU C (Alama 20)**  
**UTUNGAJI**  
Jibu swali la **saba (7)**.

7. Andika insha ya maneno yasiyopungua 350 na yasiyozidi 400, kuhusu jitihada za serikali ya Tanzania katika kuleta maendeleo kwa wananchi na uoneshe changamoto zinazokwamisha jitihada hizo.

**SEHEMU D (Alama 20)**  
**MAENDELEO YA KISWAHILI**  
Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

8. Kwa kutumia hoja sita, tahhtmini mafanikio ya lugha ya Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki.
9. Kwa kutumia hoja sita na mifano dhahiri, eleza ubantu wa Kiswahili kwa kutumia uthibitisho wa kihistoria.

**SEHEMU E (Alama 20)**  
**TAFSIRI NA UKALIMANI**  
Jibu swali la **kumi (10)**.

10. Tumia hoja tatu kuonesha kufanana na hoja tatu kuonesha kutofautiana kati ya ukalimani na tafsiri.